

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu Na: +255 (028) 2227148

Nukushi: +255 (028) 2227140



Halmashauri ya Wilaya

S.L.P 20

KARAGWE

Barua Pepe: ded@karagwedc.go.tz
utumishi@karagwedc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KGR/HWK/T.10/VOL.XVIII/12

03/08/2020

TANGAZO LA KAZI (AJIRA YA MUDA) NAFASI (10)
(TANGAZO LINARUDIWA)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anawatangazia tena wananchi wote wenye sifa za kuajiriwa katika Ajira ya Muda baada ya kupata kibali chenye Kumb Na. FA.170/368/01/110 cha tarehe 07 Mei, 2020 kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi.

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- i. Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) na awe amehitimu Astashahada ya Sheria, Utawala, Maendeleo ya Jamii, Fedha na Biashara, Uhasibu na Mipango. Kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.
- ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- iii. Awe ni raia wa Tanzania
- iv. Awe na akili timamu
- v. Awe hajawahi kushitakiwa na kufungwa kwa kosa la jinai

MSHAHARA

- i) Msahahara kwa mwezi ni TGOS A₁ yaani Tsh. 300,000/=

MAJUKUMU

- i) Kukusanya mapato ya Halmashauri kwa kutumia POS na kutoka stakabadhi kwa njia ya POS
- ii) Kukagua magari ya mizigo yanayopita kwenye kizuizi

- iii) Kuhakikisha fedha zinapelekwa Benki mara tu baada ya kukusanywa
- iv) Kuweka kumbukumbu sahihi ya magari ya mizigo yaliyopita kweye kizuizi husika
- v) Kutoa taarifa kwa Mhasibu wa Mapato kwa jambo lolote litakalojitokeza lenye dalili za uvunjifu wa sheria
- vi) Kutoa taarifa kwa Mhasibu wa mapato kwa fedha zilizokusanywa kwa siku husika

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI;-

- i) Maombi yaambatishwe na taarifa binafsi (CV) yenye anwani na namba za simu zinazotumika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu
- ii) Nakala za vyeti vya elimu na taaluma
- iii) Cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
- iv) Picha 2 (Passport size) za hivi karibuni
- v) Waombaji walostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- vi) Ajira hii ni ya kipindi cha mwaka mmoja (Bila Mkataba huo kuhuishwa)

NB: Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 20
KARAGWE.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 17/08/2020 Saa 9:30 Alasiri

Imetolewa na:



G. M. Kitonka

MKURUGENZI MTENDAJI